**NOA BONGO, JENGA MAISHA YAKO**

**"Kabumbu Afrika - Ni zaidi ya mchezo!"**

## KIPINDI CHA TISA: "Wajenzi na waharibifu"

MWANDISHI: Chrispin Mwakideu

WAHARIRI: Andrea Schmidt,Thelma Mwadzaya

Orodha ya washiriki / KIPINDI CHA TISA:

- Msimulizi

### SCENE ONE: AT MAKEMBA'S RESIDENCE

- Jonathan (mume,15)
- Mhe. Makemba (mume, 55)

### SCENE TWO:AT AUNT LILY'S

- Safina (Mke,13)
- Shangazi Lily (Mke, 33)

### SCENE THREE: TAMBARARE POLICE STATION

- Chedede (mume,14)
- Komora (mume,14)
- Inspekta Tino (mume,40)

### SCENE FOUR: MATCH AT CITY STADIUM

- Chedede (mume,14)
- Metogba (mume, 28)
- Sauti mchanganyiko za wasichana na wavulana(13+)
- Mhe. Makemba. (mume,55)
- Shangazi Lily (mke, 33)
- Mtangazaji

**INTRO**

1. **NARRATOR:** Hamjambo na karibuni tena katika kipindi hiki cha Noa Bongo, Jenga Maisha Yako, huku tukiendelea na makala ya "**Kabumbu afrika - Ni zaidi ya mchezo!**".Katika kipindi kilichopita, mchezaji wa maarufu wa kandanda Metogba aliwashauri vijana kuhusu athari za madawa ya kulevya na pombe katika michezo. Yeye na bwana Wakasa, mwenyekiti wa Shirikisho la Soka, pia waliwaeleza kuhusu mechi ijayo ya kirafiki kati yao na timu ya Tambarare. Mhe. Makemba alikamatwa na kuachiliwa kwa dhamana naye Chedede aliachiliwa na kujiunga tena na wenzake katika kliniki ya soka. Ni yapi yatakayotokea leo? Baki nasi hadi tamati ili uwabaini "**Wajenzi na waharibifu"**. Tunalifungua jamvi letu katika makazi ya Makemba.

**SCENE ONE: AT MAKEMBA'S RESIDENCE**

2. **MHE. MAKEMBA:** Jonathan, Nisikilize mwanangu, yote niliyoyafanya ni kwa manufaa yako... bado u mtoto huelewi mambo yalivyo.

3. **JONATHAN:** Udogo wangu si hoja... naelewa kila kitu. Ulichokifanya si sahihi. Ulinieleza kuwa, kabumbu huchezwa kwa miguu, kichwa na kifua, sio kwa pesa zinazo hujumu, kusaliti na kukandamiza.

4. **MHE.MAKEMBA:** Nilitaka wewe uwe mchezaji bora zaidi! **(Shouts** ) na bado nitakuja kwenye kinyang'anyiro hicho leo kukushangilia.

5. **JONATHAN:** **(Shocked)** Nini? !!! Baada ya ulichokifanya?! Utawezaje kuwatazama walimwengu baada ya yote hayo?

6. **MHE.MAKEMBA: (Sarcastic)** Taratibu. Mimi ni mtu wa watu.Ni mtumishi wa umma. Umma unanipenda. Haya mashtaka yatatupiliwa mbali. Kauli zangu ndizo zitakazoaminika sio za chokoraa fulani kutoka Tambarare. Unadhani mahakama itamuamini nani kati yetu?

7. **JONATHAN: (Sarcastic)** Kumbe ni hivyo? Basi utashangaa Baba. Tamko lako litakuwa dhidi ya timu nzima na mimi pia. Niliusikia ushahidi kuwa ulishirikiana na Komora katika njama hii ya wizi na kisha ukamsingizia Chedede. Kwa kifupi kauli zako zitakuwa dhidi ya umma. Mimi naenda uwanjani kwenye mechi sasa.

8. **MHE.MAKEMBA:** Ngoja ntakupeleka kwa gari...

9. **JONATHAN: (Almost in tears)** Hata usihangaike Baba, ulikuwa mfano kwangu, nilitaka kukushabihi, nizungumze kama wewe, matendo yangu yawe kama yako, hata nicheze kama wewe. nilifikiri ulikuwa shabiki wa soka kumbe wewe ni adui wa soka. Umenivunja moyo. Kwa heri.

10. **SFX: DOOR BANGS SHUT.**

11. **NARRATOR:** Jonathan alikuwa analengwalengwa na machozi alipoondoka kuelekea kiwanjani.Alivunjwa moyo sana na babake. Wakati huohuo, Safina na Shangazi Lily walikuwa wanamaliza mlo wao wa mchana nyumbani mwake.

**SCENE TWO: AT AUNT LILY'S PLACE**

12. **SFX: CUTLERY SOUNDS AS WHEN PEOPLE EAT**

13. **SHANGAZI LILY: (Laughs out loud)** Safina, eti ulifikiri kazi yangu ni gani?

14. **SAFINA: (Also laughing)** Unaweza kunilaumu shangazi ? Niliaibika sana uliponiambia kuwa ni mhudumu wa hoteli… ila sielewi. Kwa nini lazima muvae viguo vifupi hivyo?

15. **SHANGAZI LILY:** Kwa sababu mwenye hoteli alisema nguo hizo huwavutia wateja sana, na ni kweli. Mimi hujipatia marupurupu mengi hata kuliko mshahara wangu. **(Chuckles)** Safina, basi fanya haraka usichelewe uwanjani.

16. **SAFINA:** Shangazi Lily, nafurahi sana kuwa unakuja kuitazama mechi yetu. Awali nilidhani huipendi soka lakini sasa nimetambua kuwa kweli wewe ni shabiki na rafiki wake.

17. **SHANGAZI LILY:** Nyinyi ndio mumenifanya nikabadili mtazamo. Wewe, Chedede, Metogba na wengineo. Sasa kajitayarishe, nitamaliza kuosha vyombo. Umeshafanya kazi ya kutosha.

18. **SFX: PLATES AND SPOONS BEING CLEARED.**

19. **NARRATOR:** Safina anapojitayarisha kwenda mpirani, Dede alikuwa amewasili kwenye kituo cha polisi kumtembelea rafiki yake Komora, ambaye sasa amegeuka adui.Tega sikio.

**SCENE THREE: POLICE STATION TAMBARARE CITY**

**20. SFX: METAL DOOR BEING UNLOCKED**

**21. INSPEKTA TINO:** Unaa...

**22. CHEDEDE:** Dakika tano, na huku ndani ni Sawa na dakika mbili na nusu.

**23. INSPEKTA TINO:** Kumbe unakumbuka. Haya nitawaacha muongee.

**24. CHEDEDE:** Vipi, Komora.

**25. KOMORA: (Indifferent)** Wataka nini kutoka kwangu Dede, umekuja kunikejeli sio?

**26. CHEDEDE:** La, siwezi kufanya hivyo. Nimekuja kukuarifu kuwa ile mechi muhimu inachezwa hii leo.

**27. KOMORA:** Najua, maafisa wote wa polisi wanaizungumzia. Kwa hivyo umekuja kutafuta kuungwa mkono na mimi? Sivyo? **(Hatefully)** Natumai mutashindwa! Natumai uvunjwe mguu na usicheze tena kabumbu. Kandanda sio mchezo muhimu. Hicho ndicho kilichonifanya nizuiliwe humu ndani.

**28. CHEDEDE:** Nakuhurumia, Komora. Tena sana, ni dhahiri hukuwa rafiki wa dhati. Uliuonea wivu ustadi wangu, na hata baada ya uovu wote ulionitendea bado una kinyongo na mimi. Soka inapaswa kuwaunganisha watu,kuwaleta pamoja watu wa kusini na kaskazi, mashariki na magharibi, maskini na matajiri, weusi na weupe, lakini wewe na mheshimiwa Makemba mulifanya kinyumena hilo. Kwa heri Komora.

**29. KOMORA: (Shouting)** Mutafungwa! Dede... Hutafaulu. Ulitoka mapipani na utabaki mapipani ukiombaomba!

**30. INSPEKTA TINO:** Kimya!

**31. SFX: METAL DOOR BEING LOCKED.**

**32. NARRATOR:** Kabumbu barani Afrika ni sehemu ya maisha. Baadhi wanaiona kama ibada. Si jambo la kushangaza kuwa mchana huo, uwanja ulijaa mashabiki. Hata mheshimiwa raisi alikuwapo kushuhudia mchuano huo. Mhe. Makemba alipokuwa anaelekea kwenye jukwaa la wageni wa heshima, aliiona sura aliyoikumbuka vyema.

**<u>SCENE FOUR:MATCH AT CITY STADIUM</u>**

**33. SFX: CHANTS /CHEERS FROM FOOTBALL FANS, SONGS.**

**34. Mhe. MAKEMBA: (Aloud)** Lily!.. Lily!.. ni wewe? Unapendeza ajabu. Muda mrefu sana tangu tuonane, ni miaka mingapi vile?

**35. SHANGAZI LILY: (Painfully)** Hilo halitobadili kitu Makemba.
Kwa nini uniulize wakati huu? Unataka kujua ni muda gani uliopita? Imepita

miaka 15. Miaka kumi na tano ya shida na dhiki...

**36. Mhe. MAKEMBA:** Samahani Lily. Nilikuwa kijana, mjinga na mwoga.

**37. SHANGAZI LILY: (Angry)** Hata haya huna. Mimi je? Nilikuwa na miaka kumi na nane! Uliniacha wakati nilikuhitaji sana.

**38. Mhe. MAKEMBA:** Lily, huyajui majuto niliyo nayo kwa sababu ya matendo yangu. Nieleze, yalikusibu yapi..... baada ya…

**39. SHANGAZI LILY:** Nilifanya lililohitajika... mechi iko karibu kuanza. Sitaki kuikosa sehemu yoyote.

**40. SFX: CHANTS AND CHEERS FROM FANS.**

**41. METOGBA:** Leo ni leo, asemaye kesho ni muongo! Tambarare F.C. ni timu ilio na uzoefu, lakini kumbukeni, mpira ni mviringo na unadunda kwa kila mmoja. Kuweni makini, shirikianeni na iwapo tunashinda au kushindwa, la msingi ni furahieni mechi. Na kabla sijasahau, wakala wa soka yumo humuhumu, sasa twendeni, twendeni!!!

**42. SFX: WILD CHEERS/BOOS THEN WHISTLE BLOWS…..CHANTS CONTINUE IN BACKGROUND**

**43. NARRATOR:** Mchuano huo ulitangazwa moja kwa moja kwenye vituo vya redio na televisheni kwa sababu Raisi alihudhuria. Chedede alidhani kama ni ndoto alipouona umati mkubwa uliokusanyika kwenye uwanja wa michezo kumtazama nani? Raisi! Alijiahidi moyoni na haikuchukuwa muda mrefu kuwa kweli, tuone hayo tukimpa usukani mtangazaji!

**44. COMMENTATOR:** Tuko katika dakika ya tano, Kama umejiunga nasi sasa unashuhudia "Mchuano dhidi ya Daudi na Goliati" kama wasemavyo waandishi wa habari.Mabingwa wa mwaka uliopita Tambarare F.C,wanachuana na wachezaji chipukizi wa soka walioandaliwa na Metogba. Kwa sasa timu ya vijana imejitahidi kwa ulinzi mkali **(Excited voice)** Jonathan anapewa pasi ya nguvu pale! na...

**45. SFX: BALL KICKED HARD:PUNCHED AWAY BY GOALKEEPER.**

**46. COMMENTATOR:** Loh! tulikuwa tumehesabu bao! Mkwaju sambamba kutoka kwa Jonathan Makemba lakini ukaokolewa na mlinda lango wa Tambarare F.C..kona ya kwanza ,amini usiamini vijana hawa wanafanya mashambulizi!

**47. SFX: WHISTLE BLOWS. BALL KICKED.**

**48. MTANGAZAJI:** Wasikilizaji mpira unakuja huo......

**49. SFX: BALL HEADED IN.WHISTLE BLOWS AGAIN.**

**50. COMMENTATOR:** Baaaaoooooooo! Wavu umetikiswa!.kichwa safi kutoka kwa chipukizi, Chedede. Tambarare F.C. haiamini yaliotokea...

**51. SFX: WILD CHEERS AND BOOS GROW LOUDER**

**52. COMMENTATOR:** Mashabiki wa Tambarare, hawakuufurahia uamuzi wa mpiga kipenga … baadhi wanaanza kurusha chupa na mawe uwanjani. Mambo yanakwenda mrama hapa uwanjani. Raisi huyo anaondolewa na walinzi wake uwanjani. Muamuzi pia ameondoka uwanjani.Ni vurugu kila mahali uwanjani... kuna mshikemshike kwani kila mtu anajaribu kutoka nje na polisi wanafyatua mabomu ya gesi ya kutoa machozi kuwatawanya wahalifu.

**53. SFX: POLICE SIRENS,NOISY CROWD**

**54. METOGBA: (Shouts )** Chedede, wahimize wachezaji wote waondoke uwanjani, twendeni kwenye chumba cha kugeuzia sare.

**55. CHEDEDE: (Shouts)** oye! Jamaa! Metogba amesema twende kwenye chumba cha kugeuzia sare...

**56. SFX:NOISE FROM THE STADIUM FADING OFF**

**57. COMMENTATOR:** Aibu tupu**.** Ni jambo la kusikitisha kuwa mechi hii imesimamishwa kwa sababu ya mashabiki wachache ambao hawakuridhika, na hawakubali kushindwa. La kweli ni kuwa hili halitoifanya soka nchini humu kuimarika. Hawa ndio maadui wa soka. Ni wajibu wa Bwana Wakasa na Shirikisho la Soka kuwaadhibu wahusika. Sasa turudi studio....

**58. SHORT MUSIC INTERLUDE**

**OUTRO:**

59. **NARRATOR:** Na mpaka hapo nipo tumefikia tamati ya kipindi cha tisa cha, "**Kabumbu Afrika - Ni zaidi ya mchezo!**". Je, shangazi Lily atafanikiwa kuondoka uwanjani akiwa salama salmin? Ni siri gani aliyomficha mhe. Makemba kwa miaka 15? Metogba atamteua nani kuwa mchezaji bora atakayepata mkataba wa timu yake ili acheze barani Ulaya? Wakala naye atamchagua nani apewe mkataba ule mwengine? Yote haya yatajibiwa katika kipindi kifuatacho. Ukitaka kusikiza tena kipindi hiki au chochote kilichotangulia tembelea kurasa zetu za tovuti www.dw-world.de/lbe. Mpaka tutakapokutana tena. Kwa heri.